Tangazo la Serikali Na. 332 la tarehe 21/8/2015

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA 290)

---

# SHERIA NDOGO

---

*Zimetungwa chini ya kifungu 6(1) na 16(1)*

---

## SHERIA NDOGO ZA (KODI YA MAJENGO) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA BUKOBA ZA MWAKA, 2015

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za(Kodi ya Majengo) Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba, 2015.

Eneo na tarehe ya kuanza kutumika

2. Sheria Ndogo hizi zitaanza kutumika katika eneo lote la Halmashauri kuanzia tarehe ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:

'' Halmashauri'' maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba;

'' Mkurugenzi'' maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba au Afisa yeyote aliyeidhiniwa kufanya kazi kwa niaba ya Mkurugenzi;

''Majengo'' maana yake ni uzio, msingi, ghati, mnara, jengo la makazi, biashara au kiwanda ambalo ujenzi unaendelea, au umekamilika na lipo katika maeneo yaliyopimwa au ambayo hayajapimwa;

''Wakala'' maana yake ni mtu au kampuni iliyoteuliwa na Halmashauri kukusanya ada ya majengo kwa niaba ya Halmashauri;

''Kodi ya jengo'' maana yake ni fedha zinazolipwa na

mmiliki wa jengo au mwakilishi wake katika Halmashauri;

''Mmiliki wa jengo'' maana yake ni mtu au taasisi, inajumuisha pia shirikalolote lililo na jengo ndani ya mamlaka ya Halmashauri.

Ushuru wa majengo

4. (1) Mmiliki wa jengo atawajibika kulipa kodi ya jengo kwa wakala au mtoza ushuru mara moja kwa mwaka kama ilivyoainishwa katika sehemu ya jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi kwa eneo husika.

(2) Endapo mmiliki wa jengo atashindwa kulipa kodi ya jengo kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, Halmashauri itampelekea hati ya madai kwa hati maalum iliyotayarishwa na Halmashauri, iliyoainishwa katika jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi, ikimtaka kulipa kodi hiyo ndani ya siku kumi na nne toka tarehe ya hati ya madai.

Cap 289 R.E, 2002

(3) Endapo hati ya madai imetolewa chini ya kifungu kidogo cha 2 cha kifungu hiki na mmiliki wa jengo akashindwa kulipa kodi ya majengo ndani ya muda atakaokuwa amepewa; itakuwa ni halali kwa Mkurugenzi, kutoa hati kwa dalali wa mahakama, kama ilivyo katika jedwali la tatu la Sheria Ndogo hizi linalosomeka na kifungu cha 43 cha Sheria ya Kodi ya Mamlaka za Miji cha kuamuru akamate mali ya mmiliki wa jengo yenye thamani ya kodi ya jengo inayodaiwa kama ilivyoainishwa katika jedwali la tatu la Sheria Ndogo hizi. Isipokuwa, hati hiyo haitatolewa hadi hati ya madai chini ya kifungu cha 2 itakapokuwa imetolewa na kupokelewa na mmiliki wa jengo, au imewasilishwa kupitia sehemu yake ya kazi au makazi yake na kupewa yeye au mkaazi wa nyumba yake aliye na umri kuanzia miaka 18 na kuendelea, au imepitia ofisi yake na kupokelewa na yeye mwenyewe au wakala wake.

Muda wa kulipa kodi ya jengo

5. (1) Tarehe 30 ya mwezi Aprili kila mwaka itakuwa siku ya mwisho kwa kila mmiliki wa jengo kuwa amelipa kodi kwa Halmashauri.

(2) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, majengo yanayomilikiwa na Serikali Kuu na nyumba za ibada zilizo rasmi, hazitahusika katika ulipaji wa kodi ya majengo.

(3) Katika kuondoa shaka, majengo yote ya Serikali yaliyonunuliwa na watumishi wa Serikali au mtu mwingine yeyote anayetambuliwa kwa mujibu wa sheria, yatatozwa kodi ya majengo.

Uteuzi wa Wakala Sheria No. 21 ya 2004

6. (1) Halmashauri inaweza, kwa utaratibu wa zabuni chini ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya 2004, kumteua mtu yeyote, kampuni binafsi au taasisi kuwa wakala wa kukusanya kodi ya majengo kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kusitisha na kubatilisha uteuzi wowote wa wakala endapo itathibitishwa kuwa wakala amekiuka Sheria Ndogo hizi au sheria yoyote ya nchi kuhusiana na uwakala wake.

Makosa

7. Itakuwa kosa kwa mtoza ushuru yeyote au wakala endapo:-

(1) Atashindwa/ataacha kutoa taarifa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

(2) Atashindwa/ataacha kuwasilisha makusanyo ya kodi aliyokusanya au;

(3) Atashindwa/ataacha kuwasilisha kodi aliyokusanya kwa mujibu wa viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hizi; au

(4) Atashindwa/ataacha kuweka kumbukumbu au taarifa za makusanyo ya kodi ya majengo, au

(5) Akitoza kodi nje ya viwango vilivyoainishwa;

Adhabu

8. Mtu yeyote atakayevunja Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo cha miezi kumi na miwili jela au vyote viwili yaani kifungo na faini.

Kufutwa Sh( Ndogo

9. 'The Bukoba Town Council (Property Rates) By Laws of 2005' zimefutwa isipokuwa madeni yote yanayotokana na Sheria Ndogo hizo yataendelea kudaiwa chini ya Sheria Ndogo hizo na kuchukuliwa kuwa hazijafutwa.

**JEDWALI LA KWANZA**

*(Chini ya kifungu cha 4(1))*

**USHURU WA MAJENGO**

**:MU A:** Jengo lolote ndani ya Manispaa lilofanyiwa uthamini litalipiwa kodi ya asilimi thamani ya jengo hilo kwa mwaka.

**:MU B:** Majengo yaliyopo katika maeneo ambayo hayakupimwa lakini hayakufanyiwa yatalipiwa shilingi elfu nane (8,000/=) kwa mwaka, isipokuwa nyumba zilizoje kwa miti na udongo.

**:MU C:** Majengo ya makazi yaliyopo katika maeneo yaliyopimwa lakini hayakufanyiw yatalipiwa kiwango cha Tsh 20,000/= kwa mwaka.

**:MU D:** Majengo ya biashara na taasisi katika maeneo yote lakini ambayo hayajafanyi\ yatalipia viwango vya ada ya majengo vifuatavyo:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| Sehemu zote: | (i) majengo ya biashara: | Sh. 50,000/= | kwa jengo kila mwaka |
| | (ii) majengo ya taasisi: | Sh. 45,000/= | kwa jengo kila mwaka |

**JEDWALI LA PILI**

*(Chini ya kifungu cha4(2))*

HALMASHAURI YA MANISPAA YA BUKOBA (KODI YA MAJENGO)
SHERIA NDOGO ZA MWAKA, 2015

HATI YA MADAI

Kwa Bw/Bi/Bibi.....................................................................................
.....................................................................................
.....................................................................................

Pata taarifa kuwa wewe kama mmiliki wa jengo linalopaswa kulipiwa ushuru wa majengolililopo katika Kiwanja Na.................Kitalu.....................Kata ya..................... ndani ya mamlaka ya Manispaa ya Bukoba, unadaiwa jumla ya Sh. ........................................................................
zikiwa ni malimbikizo ya kodi ya majengo ambazo unapaswa kulipa ndani ya siku kumi na nne toka tarehe ya kupokea hati hii.

Tarehe:....................................	Sahihi:.......

wa H
go hiz
i ulioi

**JEDWALI LA TATU**

*(Limetengenezwa chini ya kifungu 4(3))*

HALMASHAURI YA MANISPAA YA BUKOBA (USHURU WA MAJENGO) SHERIA NDOGO ZA MWAKA, 2015

*(Limetengenezwa chini ya kifungu Na. 4(3))*

Kwa Dalali wa Mahakama,
…………………………….
…………………………….

Unaamriwa kukamata na kushikilia mali inayohamishika/isiyohamishika inayomilikiwa na Bw/Bibi/………………………………………………………… ………………………………………………………………………………… ………………………………………………………………………………… kama inavyoonyeshwa katika orodha ya kiambatanisho, na kuwa isipokuwa Bw/ Bibi/………………………….. atakuwa amelipa kiasi cha Shilingi……………… ………………………………………………………………………………… pamoja na riba ya silimia moja kila mwezi kuanzia tarehe…………….mwezi wa…………………………………………………………………………………… pamoja na gharama za utimizaji wa amri hii, na baada ya kutoa taarifa ya siku 14 kwa kubandika taarifa hiyo katika jengo la mahakama hii, mali hiyo itauzwa kwa mnada ili kukomboa deni, riba na gharama za utimizaji wa amri hii, kama ilivyoelezwa ndani ya hati hii. Unaamriwa vile vile kurudisha hati hii katika mahakama hii ikiwa na maelezo namna amri hii ilivyotimizwa au isivyowezekana kutimizwa mnamo au kabla ya tarehe……………………….. Imetolewa kwa amri yangu na mhuri wa mahakama, hii leo, tarehe……………………………….20…..

…………………………

**Hakimu wa Wilaya**

Nembo na muhuri wa Halmashauri ya Manispaa Bukoba umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kwa Azimio [illegible] na Mkutano wa Baraza la Madiwani ulioitishwa tarehe 05 mwezi 12 na ubandikwaji huo kushuhudiwa na:-

....................................

**CHIBHUNU LUKIKO**
*Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba*

....................................

**MH. ALEXANDA NGALINDA**
*Naibu Meya Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba.*

NAKUBALI,

....................................

**MH. MIZENGO P. PINDA (MB)**
Waziri Mkuu.

Dodoma,
Tarehe....2/7/6/2015....